


Lengo siyo Idadi tu ya Wanafunzi, Bali ni Ubora wa Elimu: Sekta ya Elimu & Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Bajeti ya 2009/2010

Lengo la muhtasari huu ni kuwasaidia wabunge na wananchi ili waweze kuelewa vizuri na hatimae kuchangia katika bajeti ya wizara ya elimu ya mwaka wa fedha 2009/10 ambayo itasomwa bungeni tarehe 23/7/2009.

Maendeleo ya jamii yoyote ile hutegemea sana elimu. Elimu ni haki ya kila mtu, wakiwemo watoto wetu. Sisi sote, wazazi, jamii na serikali kwa ujumla tunao wajibu wa kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata elimu bora na si bora elimu kama ilivyo hivi sasa. Elimu bora ni ile inayomwezesha kila mtu awe na uwezo wa kufikiri kwa makini, kuwa mbunifu na kuwa na uwezo wa kutatua matatizo yanayomkabili. Pia ni ile inayomwezesha mtu kutumia maarifa aliyoyapata kutengeneza na kutumia fursa kuji-letea maendeleo binafsi, ya familia na taifa kwa ujumla.

Elimu—Kipaumbele Namba 1ⁱ

Tunaipongeza serikali kwa kuipa kipaumbele cha kwanza sekta ya elimu. Hii inaonesha kuwa serikali inatambua umuhimu wa elimu kama kichocheo kikubwa katika mapambano dhidi ya umaskini. Katika mwaka wa fedha 2009/10 sekta ya elimu imetengewa kiasi cha shilingi **1.7 triloni**, ambayo ni sawa na **18.3%** ya bajeti yote ya serikali. Hii ni sawa na ongezeko la 21% ikilinganishwa na ile ya mwaka uliopita. Jedwali namba 1 linaonyesha mwenendo wa bajeti ya elimu katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.




Jitihada hizi zote zinalenga kuimarisha sekta ya elimu nchini. Kwa kiasi kikubwa tumefaulu kuongeza uandikishaji wa wanafunzi shuleni. Kwa sasa zaidi ya 97% ya watoto wa umri wa kwenda shule ya msingi wako shuleni. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa watoto wote wanaopaswa kuwa shule, wako shuleni. Hata hivyo mafanikio haya bado hayatoshi. Tunasema hivyo kwa sababu tafiti nyingi na hata vyombo vya habari vinaonesha kuwa bado kuna upungufu mkubwa wa walimu, maabara, madarasa pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Ni elimu ipi iliyobora itakayopatikana bila maabara, madarasa, vitabu na walimu wa kutosha? Je katika hali hii, lengo la kuwapatia elimu bora watoto wetu litafikiwa?

Wakati tunaipongeza serikali kwa kuongeza bajeti ya elimu katika mwaka wa fedha 2009/10, ni vema basi katika bajeti hii, kipaumbele kikawa kuboresha elimu.

Bajeti Inaongezeka lakini Ruzuku ya Wanafunzi Inapunguaⁱⁱ

Ili kuboresha elimu ya msingi, utoaji wa ruzuku ya wanafunzi (capitation grant) ni jambo la msingi. Ruzuku ya wanafunzi ni pesa inayotoka serikalini kwa ajili ya kila mwanafunzi aliye katika shule ya msingi. Ruzuku hii ilianzishwa mwaka 2001 wakati serikali ilipoamua kuondoa ada na michango katika shule za msingi nchi nzima na kutoa ruzuku ili itumike kununua mahitaji ya wanafunzi kama vile vitabu, madaftari, kalamu na pia kufanyia ukarabati mdogo wa majengo ya shule.

Cha kushangaza ni kwamba wakati bajeti ya elimu inaongezeka, ruzuku hii imekuwa inashuka kila mwaka. Kwa mfano mwaka 2001/02, ruzuku ya wanafunzi ilikuwa shilingi **13,000** (dola 10 Merekan) kwa kila mwanafunzi. Mwaka 2007/08, ilipungua na kuwa shilingi **10,000**. Na katika bajeti ya mwaka huu 2009/10, itapungua na kufikia shilingi **8,000**. Ni wazi kuwa kupungua kwa ruzuku hii kutaathiri upatikanaji wa elimu bora ya msingi.



Mabadaliko Makubwa katika Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Matumizi ya Kawaidaⁱⁱⁱ

Matumizi ya kawaida katika bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yameshuka kutoka shilingi 397,889,941,300 mwaka 2008/09 hadi kufikia shilingi **377,691,167,000** katika mwaka 2009/10.

Kwa kuangalia kiwango cha kushuka huku kwa bajeti ya Wizara ya Elimu ukilinganisha na ile ya mwaka uliopita, mtu anaweza kusema kuwa kumekuwepo na kupunguzwa kwa bajeti katika idara zote za wizara husika, lakini siyo hivyo. Ukweli ni kwamba imependekezwa kuwa bajeti za idara zote iongezwe isipokuwa ile ya idara ya Elimu ya Sekondari ambayo imepunguzwa sana. Kwa jumla, ukiondoa bajeti ya idara ya Elimu ya Sekondari, uta-

ona kwamba bajeti ya Wizara imeongezeka kwa shilingi **bilioni 45**, au **16% zaidi** ya ile ya mwaka uliopita.

Mwaka uliopita idara hii ya Elimu ya Sekondari ilitengewa shilingi bilioni 108, lakini mwaka huu imepunguzwa kwa kiasi kikubwa cha fedha kwa kutengewa shilingi **bilioni 2 tu**. Swali tutanalojiuliza ni kwamba je umuhimu wa shughuli za idara hii umepungua kiasi hicho hata kuwa na bajeti ndogo kama hii au shughuli zake zimepelekwa katika idara zingine?

Sisi kama walipa kodi tunaumizwa na kukerwa na matumizi mabaya ya fedha yanayotokana na kodi zetu. Moja ya maeneo ambayo tunadhani fedha zetu zinatumika vibaya ni malipo ya posho, mafuta, na safari. Tunaipongeza serikali kwa kupunguza fedha za mafuta na safari; tunaomba pia iangalie uwezekano wa kupunguza posho mbalimbali ambazo katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka huu zimeongezeka mara mbili zaidi.

Jedwali 3: Matumizi ya Kawaida (Bilioni ya Shilingi)

	2008/09	2009/10
Posho	2.4	6.4
Mafuta	3.4	1.6
Safari	18	6.7

Matumizi ya maendeleo^{iv}

Bajeti ya matumizi ya maendeleo kwa mwaka huu ni karibu sawa na bajeti ya mwaka jana. Lakini kuna mabadiliko makubwa katika mipango michache muhimu.

Jedwali 4: Matumizi ya Kawaida (Bilioni ya Shilingi)

	2008/09	2009/10
Programu za Maendeleo ya Sekta ya Elimu (EDSP)	0.2	3.2
Ukarabati wa Majengo ya Shule/Vyuo na Ofisi	1.6	4.0
Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Elimu	0.8	3.5
Mipango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM)	8.1	3.8
Mipango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES)	3.5	0.5
Uendeshaji na Usimamizi wa Elimu ya Sekondari	20	0
Kutegemeza Elimu Maalum	0.5	0
Elimu ya UKIMWI	0.3	0

Kama inavyooneshwa katika jedwali namba 4 hapo juu, kumeuwepo na ongezeko la bajeti katika baadhi ya maeneo, kwa mfano katika mipango ya Ukarabati wa Majengo ya Shule na TEHAMA. Kwenye mipango hii, madarasa na maabara yataendelea kujengwa, idadi ya compyuta na vifaa vya TEHAMA itaongezeka, na mafunzo ya TEHAMA yataendeshwa. Hii ina maana kwamba elimu ya sayansi itaboreshwa zaidi.

Ni kweli kwamba fedha za mipango hii zimeongezeka kwa shilingi **bilioni 5.1**, lakini mpango wa Uendeshaji na Usimamizi wa Elimu ya Sekondari uliokuwa na bajeti kubwa ya shilingi **bilioni 20** mwaka uliopita hautatekelezwa kabisa katika mwaka huu wa fedha. Mpango huo ulihusika sana na ujenzi wa madarasa, maabara, na nyumba za walimu. Licha ya kwamba serikali haijatangaza fedha kwa ajili ya mpango huu, tunatarajia kuwa serikali itatumia namna nyingine kutekeleza mpango huu.

Pia, kitendo cha kupunguza bajeti ya mipango ya MMEM na MMES kama ilivyo sasa kinakwenda kinyume na lengo letu la kuboresha elimu. Sisi sote tunatambua umuhimu wa mafunzo ya ualimu katika uboreshaji wa elimu, lakini kuna upungufu mkubwa katika eneo hilo. MMEM na MMES ni vyanzo vikuu vya mafunzo ya walimu wa shule za msingi na sekondari. Bajeti za MMEM na MMES zikipunguzwa kama ilivyo sasa itapunguza juhudi zetu za kuboresha elimu ya watoto wetu. Tunachojiuliza ni kwamba kama fedha za sekta ya elimu zipo, kwa nini hazijawekwa kwenye mipango itakayosaidia kuleta elimu bora?

Tufanyeje Tarehe 23 Julai?

Ni wazi kuwa mapungufu yaliyomo kwenye bajeti ya elimu hasa ruzuku ya wanafunzi, ujenzi wa madarasa na maabara, na mafunzo ya walimu yana athari kubwa katika kuboresha elimu yetu. Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itawasilishwa na kujadiliwa bungeni kuanzia tarehe 23 Julai. Hivyo tunaomba wabunge ambao ndio wawakilishi wetu kufanya utetezi na kuomba ufafanuzi wa mapendekezo yafuatayo:

- Kuongeza ruzuku ya wanafunzi toka shilingi 8,000 hadi shilingi 13,000 au zaidi.
- Kuongeza fedha kwenye MMEM na MMES.
- Bajeti ya posho ipunguzwe.
- Ufafanuzi wa kina kama programu ya Elimu ya Sekondari imefutwa au iko chini ya wizara nyingine.

ⁱ Taarifa zote za sehemu hii zimetoka katika *Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi Mhe. Mustafa Haidi Mkulo (MB.)*, Kiwalisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010 na *Rapid Budget Analysis for Annual Review 2008 Education Sector*

ⁱⁱ Taarifa zote za sehemu hii zimetoka katika *Ripoti ya Utendaji wa PEDP II 2008/09*, PMO-RALG na MoEVT

ⁱⁱⁱ Taarifa zote za sehemu hii zimetoka katika *Volume II Estimates of Public Expenditure Consolidated Fund Services (Section I) and Supply Votes (Ministerial) for the year from 1st July, 2009 to 30th June, 2010 As Submitted to the National Assembly*, URT

^{iv} Taarifa zote za sehemu hii zimetoka katika *Volume IV Public Expenditure Estimates – Development Votes (Part – A) Ministerial and Regional Development Programmes for the year from 1st July, 2009 to 30th June, 2010 As Submitted to the National Assembly*, URT